**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2023/2024

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W), mwingi wa rehema mwenye kurehemu kwa kutujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana tena siku ya leo ili kutekeleza majukumu yetu ya Kikatiba ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Natoa shukuran zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipa fursa hii kusimama mbele ya Baraza lako kwa niaba ya Kamati ya Bajeti kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Mwelekeo wa Hali Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Hotuba hii ni Matakwa ya Kanuni ya 93(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la Mwaka 2020) ambayo imeelekeza kuwa, Mapendekezo ya Mwelekeo wa Mpango wa Taifa yawasilishwe katika Kamati ya Bajeti kabla ya kuwasilishwa Barazani.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nikuarifu kuwa Kamati yangu imeitekeleza vyema Kanuni hiyo kwa kupokea waraka huo na kufanya majadiliano na Afisi ya Rais - Fedha na Mipango. Aidha, katika utekelezaji wa kazi hiyo Kamati yangu pia imezingatia matakwa ya Kanuni ya 93(4) inayoelekeza Kamati ya Bajeti kuwaalika Wenyeviti wa Kamati za kudumu pamoja na Wadau kwa ajili ya kutoa maoni yao kuhusu taarifa hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa naomba niwashukuru Wenyeviti wa Kamati za

Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano wao waliyoipatia Kamati ya Bajeti kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao. Aidha, kwa namna ya kipekee kabisa naomba niwashukuru wadau mbali mbali walioalikwa na Kamati yangu kwa kutenga muda wao na kufika mbele ya Kamati kutoa maoni yao, sisi Wajumbe wa Kamati ya Bajeti tunathamini sana michango yao. Napenda kuwahakikishia kuwa maoni na michango yao waliyowasilisha ni ya umuhimu mkubwa na imezingatiwa na Kamati yangu wakati wa kufanya majadiliano na Serikali na wakati wa kuandaa Hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kukamilika kwa Hotuba hii kwa kiasi kikubwa kumetokana na michango ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti. Hivyo, napenda kuwapongeza kwa dhati kwa mashirikiano yao yaliyopelekea kutekeleza majukumu yetu kwa umahiri wa hali ya juu. Kwa ruhusa yako naomba niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Abdulla Hussein Kombo Mwenyekiti
2. Mhe. Asha Abdalla Mussa Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed Mjumbe
4. Mhe. Issa Haji Ussi Gavu Mjumbe
5. Mhe. Miraji Khamis Mussa Mjumbe
6. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda kuishukuru Sekreteriati ya Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano mzuri na ushauri wanayoipatia Kamati. Kwa ruhusa yako naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:

1. Ndg. Asha Said Mohamed Katibu
2. Ndg. Abass Vuai Mohammed Katibu
3. Ndg. Husna Rajab Othman Katibu
4. Ndg. Shaib Fadhil Shaib Katibu

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya utangulizi huo, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye Maoni ya Kamati kuhusu Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

## TATHMINI YA MWENENDO WA HALI YA UCHUMI KWA NUSU MWAKA WA FEDHA 2022/2023 (JULAI 2022 – DISEMBA 2022)

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kwamba, hadi kufikia Disemba, 2022, Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kufikia thamani ya TZS 5,062.02 bilioni kutoka thamani ya TZS 4,780 bilioni mwaka 2021. Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar unapimwa kwa kuangalia viashiria vya hali ya uchumi. Baadhi ya viashiria hivyo ni pamoja na ukuaji wa uchumi, mfumko wa bei, mwenendo wa sarafu, uingiaji wa watalii na uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuweka mikakati ya kufikia Maendeleo ya Uchumi jumuishi na endelevu kwa kuimarisha sekta ya uvuvi, kilimo, biashara kwa kuanzisha sera ambazo zitakwenda kuimarisha sekta hizo kwa kuinua hali za wananchi kiuchumi, kuongeza uwekezaji, kukuza ajira na hatimae kuongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Mfumko wa Bei za bidhaa na huduma umepanda na kufikia wastani wa asilimia 6.6 katika kipindi cha Julai – Disemba 2022 kutoka wastani wa asilimia 2.2 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021. Kuongezeka huku kwa mfumko wa bei kunatokana na kupanda kwa bei ya mafuta na gesi asilia katika soko la dunia na pia kuathirika kwa kiasi kikubwa kwa sekta ya usafirishaji ya dunia kutokana na vita vya Ukrein na Urusi.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kudhibiti mfumko wa bei kwa haraka Serikali inapaswa kuimarisha sekta mbalimbali zitakazozalisha bidhaa kwa wingi nchini ili kupunguza kuagiza na kununua bidhaa nyingi nchi za nje hususan za chakula. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya makubaliano na SMT ili wafanyabiashara wa Zanzibar waweze kununua bidhaa hususan mchele, unga wa sembe, mafuta ya alizeti na chikichi na sukari moja kwa moja kutoka viwandani au kwa wakulima Tanzania Bara na kusafirishwa kuja Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa ruzuku kwa bidhaa ya nishati za mafuta pamoja na kupunguza viwango vya ushuru wa uingizaji wa bidhaa ya sukari kutoka asilimia 25 hadi asilimia 6. Hatua hii inasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti kasi ya ukuwaji wa mfumko wa bei.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu thamani ya nakisi ya biashara, katika kipindi cha Julai –

Disemba 2022 imeongezeka na kufikia TZS 641.9 bilioni ikilinganishwa na TZS 379.6 bilioni katika kipindi cha Julai Disemba 2021. Kuongezeka kwa nakisi ya biashara kumesababishwa na kuongezeka kwa uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi zenye thamani ya TZS 788.8 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 519.1 bilioni kwa mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, sehemu kubwa ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi unabebwa zaidi na zao la karafuu hali ambayo inapelekea kuwa na nakisi kubwa ya urari wa biashara inapotokea kushuka kwa uzalishaji na uuzaji wa zao hilo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali katika kudhibiti nakisi ya biashara iendelee kuwavutia wawekezaji ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi na kuuza bidhaa hizo katika masoko ya nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa kasi ya Uingiaji wa Watalii, imeripotiwa kwamba, idadi ya watalii walioingia nchini katika kipindi cha Julai-Disemba mwaka 2022 wamefikia watalii 345,300 kutoka watalii 205,387 katika kipindi kama hicho mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 68. Ongezeko hili limesababishwa na nchi nyingi kulegeza masharti yaliyowekwa kwa ajili ya kudhibiti kuenea ugonjwa wa UVIKO 19 ikiwa ni pamoja na kurudishwa kwa huduma za usafiri wa anga. Aidha, sababu nyengine iliyopelekea ongezeko hilo ni kuendelea kutangazwa kwa Tanzania kupitia filamu ya “The Royal Tour”.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuongeza wigo wa mapato yatokanayo na Sekta ya Utalii, Kamati inaishauri Serikali itimize kwa haraka azma yake ya kuhakikisha Sekta ya Utalii inaimarika katika kisiwa cha Pemba na kukuza uchumi wa kisiwa hicho. Jambo hili litaisaidia kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mwenendo wa Sarafu ya Tanzania, Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine Duniani imeendelea kuwa tulivu kutokana na utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti. Kamati inaipongeza Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kuwa na mashirikiano ya karibu na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) katika kudhibiti ujazo wa fedha katika Uchumi na kupunguza kasi ya mfumko wa bei kwa kutumia Sera za Kifedha na Kibajeti (Monetary and Fiscal Policies). Hatua hizi, zinasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti kasi ya kuporomoka kwa Shilingi ya Tanzania na kasi ya mfumko wa bei.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA NUSU MWAKA WA FEDHA 2022/2023 (JULAI 2022 – DISEMBA 2022)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipopitia Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023 imebaini kuwa, jumla ya TZS 1,352.19 bilioni zilipangwa kutumika katika Miradi ya Maendeleo. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2022, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023 unaonesha kiasi halisi cha fedha zilizotumika ni TZS 190.1 bilioni sawa na asilimia 70.9 ya lengo la TZS 268.0 bilioni kwa kipindi hicho na sawa na asilimia 14.1 tu ya lengo la TZS 1,352.19 kwa mwaka mzima.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/2023 umebakia muda mfupi kabla ya kumalizika, Kamati inaishauri Serikali kupanga bajeti ambazo zina uhalisia kwani kuna baadhi ya miradi inapangwa kwa miaka kadhaa lakini hakuna utekelezaji unaofanywa hata wa kazi za awali. Mathalan, katika Mradi wa Mpango wa Utayarishaji wa Matumizi ya Ardhi Zanzibar ambao ulipangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, lakini kiuhalisia mradi huu haujaanza kutekelezwa kwa sababu ndio kwanza upo katika hatua za maandalizi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali, kuijengea uwezo Tume ya Mipango, ili iweze kupanga mipango ya Serikali kwa uweledi na uhalisia, kuepuka kuingiza miradi ambayo haitatekelezeka katika muda uliyopangwa. Hii itaondosha kupandisha Bajeti ya Serikali, ambayo mara nyengine inakosa uhalisia.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA NUSU WA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 (JULAI 2022 – DISEMBA 2022)

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Julai - Disemba 2022 inaonesha kuwa, Serikali imefanikiwa kukusanya TZS 659.69 bilioni ikiwa ni asilimia 26 ya bajeti ya mwaka ya kukusanya TZS 2,572.7 bilioni. Kiasi hichi ni kidogo mno, kwani mategemeo ya makusanyo ya nusu mwaka ni kufikia asilimia 50 ya makadiro ya mwaka nzima.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine mapato yaliyokusanywa katika kipindi hicho cha Julai - Disemba 2022 yameonesha ukuaji wa asilimia 36 ikilinganishwa na

mapato ya TZS 484.67 bilioni yaliyokusanywa katika kipindi cha Julai - Disemba 2021. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hili lakini inaendelea kusisitiza kwamba fursa ya mapato bado ipo kwa kuongeza wigo wa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi Julai - Disemba 2022, mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) yamefikia asilimia 99 ya makadirio. Hatua hii ni ya kupongezwa sana lakini bado tunayo fursa kubwa ya kuongeza mapato yetu maradufu. Mathalan, miongoni mwa changamoto ambazo zinaathiri hatua za kuongeza ukusanyaji wa mapato ZRA ni kutotumika ipasavyo kwa mashine za VFMS kwa baadhi ya walipakodi wa hoteli na kuendelea kutumia mashine zao za kutolea risiti (POS). Kati ya Walipakodi wa hoteli 720 waliosajiliwa na ZRA, ni walipakodi 5 tu ndio ambao tayari wameunganishwa mifumo yao na mfumo wa VFMS waliobakia bado wanatumia POS. Serikali inapaswa kuchukua hatua za haraka za kuwafanya wawekezaji katika Sekta ya Utalii wanafuata Sheria na taratibu za nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar kwa kipindi cha Julai - Disemba 2022 yamefikia asilimia 99 ya makadirio ya kipindi hicho. Mafanikio haya ni makubwa na yanapaswa kupongezwa lakini pia bado ipo fursa kubwa ya makusanyo haya kuongezeka maradufu iwapo changamoto ya kuwepo kwa ufanisi mdogo wa bandari yetu itatatuliwa kwa haraka. Serikali inapaswa kutekeleza hatua za kuimarisha kwa haraka utendaji kazi wa bandari ya Malindi kwa kuanzisha bandari kavu (ICD) na kutumia vifaa na mifumo iliyopo sasa kwa weledi na ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi Julai - Disemba 2022, Gawio la Mashirika ya Serikali lililopokelewa ni TZS 5.3 bilioni tu kutoka mashirika yafuatayo: TZS 3.41 bilioni kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), TZS 800 milioni kutoka Shirika la Umeme (ZECO), TZS 500 milioni kutoka Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) na TZS 104 milioni kutoka Shirika la Bima Zanzibar (ZIC). Ukitizama idadi kubwa ya Mashirika ya Umma na Kampuni za Serikali tulizonazo utabaini kwamba Serikali inapoteza kiasi kikubwa cha mapato kupitia taasisi hizi. Mashirika ya Umma na Kampuni za Serikali zinazotoa gawio ni chache na hizo chache zinazotoa, zinatoa kiasi kidogo sana.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kipindi cha Julai – Disemba, 2022 makusanyo yake yamefikia asilimia 35 ya makadirio ya kipindi hicho mwaka 2021. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na uwezo mzuri katika ukusanyaji wa mapato. Mamlaka hizi hazina watendaji wenye ujuzi katika ukusanyaji mapato, kuwepo kwa uvujaji wa mapato nakadhaalika. Kwa mara nyengine, tunashauri Serikali ivipitie vyanzo vyote vya mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ifanye utafiti kwa kila chanzo ili kuweza kufanya makadirio kulingana na uhalisia wa eneo ilipo Mamlaka husika.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Disemba 2022, Deni la Taifa linalodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) limefikia TZS 331.9 bilioni na linalodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Zanzibar limefikia TZS 2,368.1 bilioni. Hii inafanya jumla ya Deni kufikia TZS 2,700 bilioni. Kuna ongezeko kubwa la Deni letu kwani kwa mujibu wa tathmini ya Deni la Taifa katika Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi Rais – Fedha na Mipango alipokuwa akiwasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka fedha 2022/2023, hadi kufikia Machi 2022, jumla ya Deni la Taifa lilifikia TZS 1,202.6 bilioni ikijumuisha TZS 310.7 bilioni Deni linalodhaminiwa na SMZ na TZS 891.9 bilioni Deni linalodhaminiwa na SMT.

**Mheshimiwa Spika,** Deni la Zanzibar bado ni himilivu lakini kasi yake ya kuongezeka ni kubwa sana. Serikali inapaswa kuchukua hatua za kupunguza kasi ya ukuaji wa deni kama vile kuongeza ukusanyaji wa mapato, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuendelea kutafuta misaada na inapobidi kukopa basi tukope mikopo isiyokuwa ya kibiashara. Aidha, Serikali ihakikishe kwamba fedha inazokopa zinaelekezwa katika miradi ambayo itachochea uchumi wa nchi yetu na kuongeza mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Misamaha ya Kodi inayotolewa na Serikali katika kipindi cha Julai - Disemba 2022 imefikia TZS 46.06 bilioni, misamaha imeongezeka kwa TZS 37.94 bilioni ikilinganishwa na misamaha ya TZS 8.12 bilioni iliyotolewa kipindi cha Julai - Disemba 2021. Malengo ya kutoa misamaha ya kodi ni kuchochea uwekezaji, kuleta unafuu kwa wanachi, kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali pamoja na kukuza sekta binafsi. Hata hivyo, Kamati imebaini baadhi ya misamaha ya kodi

inatumika vibaya au haifikii malengo iliyokusudiwa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathimini ya misamaha ya kikodi inayotolewa na kujiridhisha kwamba inaleta tija kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Hatua hii itasaidia kudhibiti matumizi mabaya ya misamaha. Aidha, misamaha ya kodi inaweza kufanywa kama vivutio vya uwekezaji kwa kupunguza kiasi fulani cha kodi inayopaswa kulipwa badala kusamehe moja kwa moja.

## TATHMINI YA MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2022/2023 (JULAI 2022 - JUNI 2023)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa mwenendo wa makusanyo, Serikali inatarajia kukusanya TZS 1,969.33 bilioni katika kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023 sawa na asilimia 77 ya makadirio. Mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 1,337.67 bilioni sawa na asilimia 98 ya makadirio ya bajeti. Aidha, Matumizi ya Serikali Kuu hadi kufikia Juni 2023 yanatarajiwa kufikia TZS bilioni 1,969.33 billioni ikiwa ni asilimia 77 ya bajeti ya mwaka ya TZS 2,572.71 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Matarajio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2022/2023 yataweza kufikiwa iwapo Serikali itaendelea na hatua za kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato na manunuzi kwa njia ya kielektroniki sambamba na kujenga nidhamu ya matumizi ya Serikali.

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2023

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2023 kasi ya Uchumi wa Dunia inakadiriwa kukuwa kwa wastani wa asilimia 2.9 kutoka wastani wa asimilia 3.2 kwa mwaka 2022. Kupungua kwa kasi ya Uchumi wa Dunia kunatokana na athari za vita vinavyoendelea baina ya Urusi na Ukrein ambavyo vimeathiri sekta mbalimbali duniani. Aidha, Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2023 na wastani wa asilimia 6.6 mwaka 2024.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na mwingiliano wa kibiashara na kiuchumi baina ya Zanzibar na nchi nyengine za dunia, Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa dunia una athari ya moja kwa moja na uchumi wa Zanzibar. Hivyo, hatua za kuimarisha uchumi wa Zanzibar zinapaswa kuwa na ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Baadhi ya hatua ambazo Serikali imepanga kuchukua ili kuimarisha uchumi wa Zanzibar katika mwaka 2023 na 2024 ni kudhibiti kasi ya mfumko wa bei, ongezeko la ukusanyaji wa mapato, kuimarisha mazingira ya biashara, usimamizi bora wa miradi pamoja na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji na kuimarisha maghala. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaweka mikakati madhubuti ili kudhibiti na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwenye hoteli na mawakala wanaoingiza watalii nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa uimarishaji wa mazingira ya biashara, Kamati inaishauri Serikali iendelee kutekeleza mikakati ya kuimarisha mazingira ya kufanya biashara ikiwa ni pamoja na kuendelea kuondoa muingiliano wa majukumu kwa taasisi za udhibiti, utoaji wa vibali na leseni pamoja na ukusanyaji wa tozo na kodi, kuondoa tozo sumbufu na kuimarisha ushirikiano wa sekta ya umma na sekta binafsi. Aidha, Serikali iimarishe majadiliano na utatuzi wa changamoto zinazoikabili sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kudhibiti Mfumko wa Bei kwa mwaka 2023 na 2024 Serikali imepanga kuendelea kutoa bei elekezi kwa bidhaa na kuzisimamia, kuendelea kutekeleza Sera za Fedha na Bajeti ili kutunza thamani ya Shilingi ya Tanzania pamoja na kusimamia upatikanaji wa mitaji na fedha za miradi ya maendeleo kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,** Mbali ya hatua hizo, Kamati pia inaishauri Serikali kuharakisha Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Samaki na Dagaa ili kuanza kusarifu samaki na dagaa na kuuza nje ya nchi. Hatua hii itasaidia kuongeza ajira. Ajira zitakazopatikana zitakuwa za moja kwa moja kiwandani na zile zitakazotokana na shughuli za uvuvi kwa vile soko la bidhaa hizo litakuwa kubwa.

## MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/2024 umepangwa kutumia jumla ya TZS 1,463.20 bilioni (ikijumuisha TZS 1,312 bilioni za miradi halisi ya maendeleo ya Serikali Kuu na TZS 7.2 bilioni za maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa) ambazo ni sawa na asilimia 53.4 ya Bajeti yote ya Serikali ya TZS 2,739.43 bilioni kwa mwaka 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Waraka wa Mpango wa Maendeleo umetaja Maeneo ya Kimkakati ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kuwa ni Kuendeleza Uimarishaji wa Miundombinu ya Bandari, Viwanja vya Ndege na Mawasiliano, Kuendeleza Uimarishaji wa Miundombinu ya Barabara, Kuendeleza Uimarishaji wa Uchumi wa Buluu, Kuimarisha Miundombinu ya Kilimo na Mifugo, Kuimarisha mazingira wezeshi ya viwanda, Kuendelea kuwawezesha Wananchi Kiuchumi, Kuendeleza Uimarishaji wa Huduma za Kijamii, pamoja na Kuimarisha Biashara na Kuendeleza Viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuimarisha Bandari ya Mkokotoni ili iweze kutumika kwa abiria wanaoenda Pemba ambapo itasaidia kuengeza ajira na kipato kwa wananchi na Serikali pamoja na kutoa unafuu kwa wasafiri wa Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Bandari ya Malindi, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatatua changamoto za bandari hiyo kwa haraka ili iweze kuhudumia meli za mizigo kwa ufanisi. Hatua hii itasaidia kushusha gharama za usafirishaji wa mizigo inayokuja Zanzibar jambo ambalo litapelekea kuimarisha biashara kwa kiwango kikubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuimarisha Vyuo vya Mafunzo ya Amali ili kuwasaidia wajasiriamali wadogo kuongeza ujuzi, vilevile Kamati inaishauri Serikali kusaidia wafugaji wa ndani na wavuvi kwa kupunguza uingizwaji kuku na samaki kutoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaishauri Serikali kuifanyia tathmini miradi ya umwagiliaji iliyokwisha tekelezwa pamoja na kuweka mikakati madhubuti ya kuanzisha viwanda vya usindikaji wa mazao.

## MWELEKEO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 unaonesha kuwa mapato ya Serikali kwa mwaka 2023/2024 yanakadiriwa kufikia TZS 2,739.43 bilioni ikiwa ni ongezeko la TZS 149.13 bilioni sawa na asilimia 6 ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2022/2023 ya TZS 2,590.3 bilioni. Aidha, matumizi ya Serikali yanatarajiwa kufikia TZS 2,739.43 bilioni

yakijumuisha matumizi ya kazi za kawaida TZS 1,265.43 bilioni na matumizi ya kazi za maendeleo TZS 1463.2 bilioni. Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea na usimamizi na udhibiti wa fedha za umma katika matumizi yake na kuhakikisha kuwa, mwelekeo huu wa matumizi, unasaidia katika kuengeza utekelezaji wa shughuli mbali mbali katika taasisi za Serikali kwa kiwango kilichopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuifanya bajeti ya mwaka 2023/2024 kuwa bajeti ya maendeleo kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kazi za maendeleo kuliko kwa ajili ya kazi za kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** Ili Serikali iweze kukusanya mapato katika mwaka wa fedha 2023/2024 kama ilivyokadiria na kuweza kutekeleza bajeti yake kwa ufanisi, Kamati inashauri kufanyika kwa tafiti za kuibua vyanzo vipya vya mapato hususan ambavyo si vya kikodi. Hatua hii itasaidia kuongeza wigo wa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, Kamati ya Bajeti kwa dhati kabisa, inaipongeza Serikali kwa jitihada zake na hatua mbali mbali wanazoendelea kuzichukua katika kufanya mapitio na tathmini Taasisi za Serikali kwa lengo la kuziunganisha taasisi zenye majukumu ya msingi na yanayowiana ili kurahisisha shughuli za Serikali. Vile vile, Kamati inasisitiza Serikali kufanya tathmini kwa taasisi zote zinazopokea ruzuku kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi katika matumizi ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeweka mikakati mbali mbali ya kuhakikisha inapata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mikopo ya ndani na nje, mikopo kutoka taasisi za kifedha, benki za ndani na nje na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kamati inaishauri Serikali wakati utakapofika wa kuchukua mikopo hiyo, kuhakikisha hatua zote zinazofaa kutekelezwa katika uchukuaji wa mikopo zinafatwa pamoja na kufanya maamuzi sahihi ya kutambua aina ya mkopo utakaochukuliwa kwa maslahi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, miongoni mwa mikakati ya kupata rasilimali fedha iliyotajwa ni pamoja na Serikali kuendelea na jitihada zake za kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa matumizi. Mifumo hiyo iliyoainishwa ni pamoja na Mfumo wa Bajeti na Matumizi (BAMAS), Mfumo wa Manunuzi (eProz), Mfumo wa Ukusanyaji Mapato Yasiyokuwa ya Kodi (ZanMalipo),

Mfumo wa Ukusanyaji VFMs na katika miradi ya Maendeleo ni Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E System).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha mifumo hiyo. Aidha, Kamati inasisitiza wasimamizi wa mifumo hiyo, kuiunganisha na mifumo ya usimamizi wa fedha nchini ili iweze kusomana na kupata taarifa za makusanyo yaliyofanyika katika taasisi mbali mbali za Serikali sambamba na kuwapa wepesi watendaji katika kupata takwimu. Aidha, kuimarika kwa mifumo katika usimamizi wa rasilimali fedha kutasaidia uwekaji wa kumbukumbu sahihi ambazo nazo ni muhimu katika upangaji wa mipango ya nchi.

## Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na maoni niliyoyatoa katika hotuba hii kuhusu Mwelekeo wa Hali Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024, sasa napenda kuchukua fursa hii kutoa maoni ya jumla ya Kamati kama ifuatavyo:

1. Kwa lengo la kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Serikali inapaswa kutatua changamoto mbali mbali zinazozikabili taasisi za umma kama vile ukosefu wa ofisi, uhaba wa fedha za Ruzuku ya matumizi mengineyo, kutoingizwa kwa kiwango kinachostahiki cha fedha za utekelezaji wa miradi na uhaba wa vyombo vya usafiri.
2. Kuna tatizo la Mashirika ya Umma na Kampuni za Serikali kutofanya vizuri na kushindwa kuchagia gawio Serikalini. Ili kuongeza mapato na kupunguza mzigo kwa Serikali, Serikali inapaswa kuweka mikakati ya kuimarisha Mashirika na Kampuni hizo.
3. Kumekuwepo na tatizo la kuchelewa kuletwa kwa Miswada ya Makadirio na Mapato ya Wizara na Serikali katika ngazi ya Kamati, hali inayochangia kutokukaa sawa kwa ratiba za Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuzisimamia taasisi zake katika kuandaa miswada hiyo kwa wakati na hatimae kuziwasilisha Barazani mapema ili kuziwezesha Kamati za Baraza kutekeleza majukumu yake kwa muda uliokusudiwa.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nimalizie Hotuba yangu kwa kukushukuru wewe binafsi, Wasaidizi wako na Watendaji wote wa Baraza, kwa mashirikiano ya karibu pamoja na miongozo mbali mbali mliyokuwa mkiipatia Kamati katika kipindi chote cha kazi za Kamati. Nawashukuru pia Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa utulivu. Aidha, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano wao na ustahamilivu wao wakati tukitekeleza majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa msingi wa taarifa hii ni kutoa picha halisi ya mwelekeo wa Bajeti ijayo na kuipa fursa Serikali kuchukua maoni mbali mbali yenye lengo la kuimarisha bajeti hiyo, ni matumaini ya Kamati yangu kuwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati yangu pamoja na ushauri utakaotolewa na Wajumbe wa Baraza lako utazingatiwa na Serikali katika matayarisho ya Bajeti ya mwaka 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako waichangie taarifa hii, ili kuipa fursa Serikali kupitia Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kuyachukua maoni na mapendekezo yao kwa lengo la kutayarisha bajeti iliyo bora na inayoakisi uhalisia na matakwa ya wananchi na ambayo inakwenda sambamba na kasi na malengo ya Serikali ya Awamu ya nane.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

Ahsante

……………………

Mhe. Abdulla Hussein Kombo,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**